





# MALKIA NYUKI

## JARIDA LA CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

## KAMPASI YA MIZENGO PINDA

Issue 1, Volume 1
01 April 2024

**YALIYOMO......................................................Uk**


Ujumbe kutoka kwa Rasi wa Ndaki........................................1

Wajumbe wa Bodi ya Ndaki..................................................2

Uongozi wa Chuo................................................................3

Wakulima mkoani Katavi wanufaika na Kampasi ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kilichopo mkoani Katavi........4

SUA yapitia mitaala ya usimamizi wa rasilimali nyuki kwa kushirikisha wadau wa elimu.................................................5

Mhitimu wa SUA - Kampasi ya Mizengo Pinda (Katavi) apata tuzo ya mwanafunzi bora jumla..................................7

Mizengo Pinda Campus Celebrates Graduates at the 42nd Sokoine University of Agriculture Graduation Ceremony...10

APIARY APPRENTICESHIP: Vilolo's hive cleaning and insect removal exercise.......................................................................11

Mafanikio ya Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) katika Kampasi ya Mizengo Pinda, Mkoa wa Katavi...........................................................................12

SUA, Kampasi ya Mizeingo Pinda, Yashiriki Kikamilifu katika Maonyesho ya 30 ya Nane Nane, Yavutia Wageni Zaidi ya 300...................................................................................15

MPC katika michezo..............................................................19

# Ujumbe kutoka kwa Rasi wa Ndaki

## Prof. Josiah Z. Katani



Karibu kwenye Jarida la Chuo kikuu cha sokoine Cha kilimo, Kampasi ya Mizengo Pinda.

Mpendwa msomaji,

Napenda kukukaribisha kwenye toleo letu la kwanza la Jarida la Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Kampasi ya Mizengo Pinda kwa mwaka 2024. Jarida hili linaelezea mambo mbalimbali yanayofanywa na kampasi yetu katika nyanja za elimu, utafiti, ushauri wa kitaalamu, na uzalishaji mali.

Kampasi ya Mizengo Pinda inatekeleza majukumu makuu matatu ya taasisi za elimu ya juu nchini, yaani kufundisha, kufanya tafiti, na kutoa ushauri wa kitaalamu. Kampasi inaendesha programu tatu za shahada, stashahada, na astashahada katika nyanja za kilimo, mifugo, maliasili, na utalii.

Mbali na shughuli za kielimu na utafiti, kampasi pia inashiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii, ikiwa ni pamoja na kuchangia damu, michezo, maonesho ya nanenane, maonesho ya nyuki, wiki ya mwanakatavi, na makongamano na warsha.

Kampasi ya Mizengo Pinda ina dhamira ya kuboresha mitaala yake na miundombinu yake ili kukidhi mahitaji ya jamii ya kisasa. Kampasi inashirikiana na wadau mbalimbali katika kuboresha mitaala yake, na inatekeleza Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) ili kuboresha miundombinu yake.

Ninapenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuanzisha vyuo kimkakati vyenye kuleta mageuzi ya kiuchumi katika sekta ya elimu na kilimo. Kampasi ya Mizengo Pinda ina imani kwamba itasaidia kuleta mageuzi ya kiuchumi katika mikoa ya nyanda za juu kusini kupitia shughuli zake za elimu, utafiti, ushauri wa kitaalamu, na uzalishaji mali.

Nawatakia kila la kheri katika usomaji wa Jarida la Mizengo Pinda Campus News.



Prof. Josiah Z. Katani
Rasi, Kampasi ya Mizengo Pinda-Katavi

# WAJUMBE WA BODI YA NDAKI



**Dkt. Tulole Lugendo Bucheyeki**
Mwenyekiti



**Dkt. Hellena M. Mushi**
Mjumbe



**Prof. Josiah Z. Katani**
Katibu



**Bi. Fortunata M. Kabeja**
Mjumbe



**Bw. Saadi S. Nyagawa**
Mjumbe



**Bw.Annan N. Bally**
Mjumbe



**Bw.William C. Bulongo**
Mjumbe

# UONGOZI WA CHUO

## KAMPASI YA MIZENGO PINDA



**Prof. Josiah Z. Katani**
Rasi wa Ndaki

Professor of Forest Resources Assessment and Management
Email: katani@sua.ac.tz
Phone: +255 252955232



**Prof. Anna N. Sikira**
Naibu Rasi wa Ndaki - Taaluma, Utafiti, na Ushauri wa Kitaaluma

Associate Professor of in Development and Strategic Studies
Email: sikira@sua.ac.tz
Phone: +255 252955233



**Prof. Jeremiah R. Makindara**
Naibu Rasi wa Ndaki - Mipango, Fedha, na Utawala

Associate Professor of Business Management
Email: makj@sua.ac.tz
Phone: +255 252955234

**WAKULIMA MKOANI KATAVI WANUFAIKA NA KAMPASI YA CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO KILICHOPO MKOANI KATAVI.**

Kampasi ya Mizengo Pinda ilianzishwa mwaka 2019 kwa lengo mahususi la kupanua taaluma na kufanya tafiti mbalimbali katika Nyanja za Kilimo na Mifugo hususani katika mikoa ya nyanda za juu kusini na maeneo jirani. Ambapo Kampasi ya Mizengo Pinda ilianza kudahili wanafunzi kwa mara ya kwanza kwa mwaka wa masomo wa 2020/2021.

Kampasi inatekeleza majukumu makuu matatu kama zilivyo taasisi nyingine zote za elimu ya juu nchini ambayo ni kufundisha, kufanya tafiti, kutoa ushauri wa kitaalamu na uzalishaji mali katika nyanja za kilimo, mifugo, maliasili na utalii.
Kampasi kwa sasa inaendesha programu tatu, moja ikiwa ni ya Shahada ya awali katika Usimamizi wa rasilimali nyuki, programu ya pili ni Stashahada katika Uzalishaji na usimamizi wa mazao na programu ya tatu ni ya Astashahada katika Uongozaji Watalii na Uwindaji wa Kitalii.

Kwa sasa kampasi hii inaendelea na Miradi miwili ya kiutafiti katika nyanja mbalimbali. Miradi hiyo ni pamoja na mradi unaolenga kutambua njia za asili zitakazosaidia kudhibiti uharibifu na upotevu wa mazao baada ya mavuno usababishwao na wadudu aina ya viwavijeshi. Mradi huu unajulikana kama (Integrated Traditional Package for Controlling Maize weevil (Stophiluszea) to reduce post harvest losses at Katavi region). Mradi mwingine wa kiutafiti umelenga kuja na njia za kitaalamu kwa kutumia TEHAMA katika uchaguzi wa mbegu bora zenye kuhimili magonjwa. Mradi huu unajulukana kwa jina la (To wards Breeding for Fall Armyworms resistant Maize varieties) A deep learning computer model for acceleration of the selection cycle). Miradi yote miwili inafadhiliwa na "SUARIS" kupitia mapato ya ndani ya Chuo.



*Mwanafunzi wa mwaka wa kwanza katika Stashahada ya Uzalishaji na Usimamizi wa Mazao akihudumia mimea ya mahindi katika jaribio dogo la mahindi katika kampasi*

Tangu ilipoanzishwa mwaka 2019, Kampasi ya Mizengo Pinda imeendelea kuboresha miundo mbinu na mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi na wafanyakazi ikiwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundo mbinu mbalimbali kama vile madarasa, mabweni, dahalia, miundombinu ya umeme na maji n.k.

Ili kuimarisha mafunzo kwa vitendo Kampasi imeanzisha Shamba darasa la mazao ya kudumu ikiwa ni pamoja na mikorosho imepandwa na mazao mengine ya msimu kama vile mahindi na alizeti hupandwa kila mwaka. Pia shamba dogo la mafunzo eneo la Kampasi ambalo husaidia mafunzo ya vitendo yatolewayo kila siku, kuna mazao mbalimbali kama mikorosho, mipapai, miembe, mahindi na mazao mengine ya mbogamboga.

## SUA YAPITIA MITAALA YA USIMAMIZI WA RASIMALI NYUKI KWA KUSHIRIKISHA WADAU WA ELIMU.

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Kampasi ya Mizengo Pinda, kilifanya warsha na wadau wa Elimu Mkoani Tabora tarehe 22.12.2023. Warsha hiyo ililenga kupitia mitaala ya Elimu ya Shahada ya Sayansi ya Usimamizi wa Rasilimali Nyuki na Stashahada ya Sayansi ya Usimamizi wa Rasilimali Nyuki. Warsha hiyo ilijumuisha wanachuo, wahadhiri, watafiti, wafugaji wa nyuki, na wadau wengine wa sekta ya nyuki.



*Mr Jackson Kizeze kutoka TAWIRI Tabora akichangia mada katika warsha ya wadau wa elimu*

Katika warsha hiyo, wadau wa Elimu walipata fursa ya kujadili mitaala ya Elimu ya Usimamizi wa Rasilimali Nyuki na Waliweza kutoa maoni yao kuhusu ubora, uhalisia, ufanisi, na changamoto za mitaala hiyo.
Baadhi ya maoni yaliyotolewa ni pamoja na Mitaala ya Elimu ya Usimamizi wa Rasilimali Nyuki inapaswa kuendana na mahitaji na mazingira ya wafugaji wa nyuki nchini Tanzania. Inapaswa kujumuisha masuala ya kisera, kisheria, kiuchumi, kijamii, na kimazingira yanayohusu ufugaji wa nyuki.
Mitaala hiyo inapaswa kuimarisha ujuzi na uwezo wa wanachuo katika kufanya utafiti, ubunifu, na ujasiriamali katika sekta ya nyuki.
Pia Mitala Inapaswa kujumuisha masomo ya nadharia na vitendo, na kuwapa wanachuo fursa za kufanya mafunzo kwa vitendo, ziara za kiufundi, na miradi ya kuhitimu.
Mitaala hiyo inapaswa kuwa na ushirikiano na wadau wengine wa sekta ya nyuki, kama vile taasisi za Utafiti, Mashirika ya maendeleo, Asasi za kiraia, na Sekta binafsi. Ambayo Inapaswa kujumuisha masomo ya Ushirikiano, Ushauri, Uhamasishaji, na Uongozi katika sekta ya nyuki.

*James V. Lyamuya kutoka TAFORI Mkoa wa Tabora akichangia katika warsha ya wadau wa Elimu iliyofanyika Mkoani Tabora.*







***Picha kusoto:*** *Bi. Monica Yesaya, katibu tawala mkoa wa Tabora.* ***Picha kulia:*** *Aliyesimama Kulia ni muhitimu wa shaada ya sayansi ya Usimamizi wa Rasilimali Nyuki Bi. Irine Shayo .*

Warsha hiyo pia iliwapa wanachuo fursa ya kutoa maoni yao kuhusu mitaala ya Elimu ya Usimamizi wa Rasilimali Nyuki. Baadhi ya maoni yaliyotolewa na wanachuo ni pamoja na Mitaala ya Elimu ya usimamizi wa Rasilimali nyuki inawapa wanachuo ujuzi na uwezo wa kufanya ufugaji wa nyuki kwa tija na faida. Wamesema kuwa wamejifunza mengi kuhusu aina, tabia, na mahitaji ya nyuki, mbinu za ufugaji wa nyuki, uzalishaji na usindikaji wa bidhaa za nyuki, masoko na biashara ya bidhaa za nyuki.

Mitaala hiyo inawapa wanachuo fursa za kujifunza kwa vitendo na kushiriki katika shughuli za ufugaji wa nyuki. Wamesema kuwa wamepata fursa za kufanya mafunzo kwa vitendo katika maabara, shamba darasa, na mashamba ya wafugaji wa nyuki. Pia, wamepata fursa za kushiriki katika ziara za kiufundi, semina, warsha, na maonesho ya ufugaji wa nyuki. Zaidi, mitaala hiyo inawakabili wanachuo kwa changamoto mbalimbali za ufugaji wa nyuki. Wamesema kuwa wamekutana na changamoto kama vile uhaba wa vifaa vya ufugaji wa nyuki, uhaba wa rasilimali fedha na watu, uhaba wa taarifa na teknolojia, uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi, ushindani na udanganyifu katika soko la bidhaa za nyuki.



*Katika picha ni washiriki wa Warsha ya kuboresha mitaala ya Elimu iliyoandaliwa na chuo kikuu cha Sokoine cha kilimo (SUA)Kampasi ya Mizengo Pinda ilifanyika Mkoani Tabora.*

## MHITIMU WA SUA – KAMPASI YA MIZENGO PINDA (KATAVI) APATA TUZO YA MWANAFUNZI BORA WA JUMLA

**Vaileth Franc Chiwango**, mhitimu wa Shahada ya Sayansi ya Usimamizi wa Rasilimali Nyuki kutoka Kampasi ya Mizengo Pinda ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), ameshinda tuzo ya Mwanafunzi Bora wa Jumla wa chuo hicho katika sherehe za arobaini za tuzo za mwaka 2023 zilizofanyika tarehe 21 Novemba 2023. Sherehe hizo zilihudhuriwa na mgeni rasmi Prof. Caroline Nombo, ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Vaileth amepata tuzo hiyo kutokana na ufaulu wake wa daraja la kwanza na uongozi wake bora katika masuala ya kitaaluma na kijamii.
"Nimefurahi sana kupata tuzo hii. Ni heshima kubwa kwangu na familia yangu. Nimejitahidi sana katika masomo yangu na shughuli zangu za kijamii. Nimepata msaada mkubwa kutoka kwa wahadhiri wangu, wanafunzi wenzangu, na marafiki zangu. Nawashukuru sana kwa kunipa moyo na kunisaidia katika safari yangu ya elimu," alisema Vaileth baada ya kupokea tuzo yake.



*Vaileth Franc Chiwango akiwa na mgeni rasmi Prof. Caroline Nombo (Katibu Mkuu - Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia)*

***"Nimefurahi sana kupata tuzo hii. Ni heshima kubwa kwangu na familia yangu. Nimejitahidi sana katika masomo yangu na shughuli zangu za kijamii. Nimepata msaada mkubwa kutoka kwa wahadhiri wangu, wanafunzi wenzangu, na marafiki zangu. Nawashukuru sana kwa kunipa moyo na kunisaidia katika safari yangu ya elimu," - Vaileth Franc Chiwango***

"Vaileth ni mwanafunzi mwenye bidii, akili, na uwezo mkubwa. Amekuwa akiongoza darasa lake kwa ufaulu wa juu na kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kitaaluma na kijamii. Amekuwa pia akifanya utafiti na kutoa huduma za ushauri kwa jamii inayozunguka kampasi yetu. Amekuwa mfano wa kuigwa kwa wanafunzi wengine na tunajivunia sana kumlea," alisema Prof. Josiah Katani, Rasi wa Ndaki ya Kampasi ya Mizengo Pinda.

"Vaileth ni rafiki yangu wa karibu na tumesoma pamoja tangu mwaka wa kwanza. Ni mwanafunzi mwenye ucheshi, urafiki, na ushirikiano. Amekuwa akinitia moyo na kunisaidia katika masomo yangu na maisha yangu. Amekuwa kiongozi bora na mshindi wa kweli," alisema Ruth Peter Msangi, mshindi mwenzake wa tuzo ya Mwanafunzi Bora wa Shahada ya Sayansi ya Usimamizi wa Rasilimali Nyuki mwaka wa tatu.

Usimamizi wa rasilimali nyuki ni mojawapo ya fani muhimu katika kilimo na uchumi wa nchi yetu. Nyuki ni viumbe muhimu katika mzunguko wa maisha ya mimea na wanyama. Nyuki hutoa bidhaa mbalimbali kama vile asali, nta, poleni, na propolis, ambazo zina faida kubwa kwa afya na lishe ya binadamu. Nyuki pia huchangia katika kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao ya chakula na biashara kwa njia ya uchavushaji.




Hivyo basi, tunahitaji kuwa na wataalamu wengi na wenye ujuzi katika usimamizi wa rasilimali nyuki ili kuhakikisha kuwa tunalinda na kutumia vyema rasilimali hii adhimu. Vaileth ni mmoja wa wataalamu hao ambao wameonyesha uwezo na ufanisi katika fani hii. Baada ya kuhitimu, Vaileth anapanga kuendelea na masomo yake ya shahada ya uzamili katika usimamizi wa rasilimali nyuki na kufanya utafiti zaidi katika eneo hilo. Pia, anapanga kuunda kampuni yake ya kutoa huduma za usimamizi wa rasilimali nyuki na kushirikiana na wakulima na wafugaji wa nyuki katika maeneo mbalimbali. Tunampongeza sana Vaileth kwa mafanikio yake makubwa na tunamtakia kila la kheri katika maisha yake ya baadaye.

Mbali na Vaileth, wanafunzi wengine pia wameonyesha uwezo mkubwa katika masomo yao na kujipatia tuzo mbalimbali. Nora Meck Mtikile, anayesoma Stashahada ya Uzalishaji na Usimamizi wa Mazao, ameshinda Tuzo ya Mwanafunzi Bora wa Mwaka wa Pili. Cosmas M. Cosmas na Salma Ramadhan Kigwangala, wanaosoma Shahada ya Sayansi ya Usimamizi wa Rasilimali Nyuki, wameshinda Tuzo ya Mwanafunzi Bora wa Mwaka wa Kwanza na wa Pili mtawalia.

Aloyse Venance Kigwa, anayesoma Stashahada ya Uzalishaji na Usimamizi wa Mazao, ameshinda Tuzo ya Mwanafunzi Bora wa Mwaka wa Kwanza, Elizabeth Fredrick Temu ameshinda Tuzo ya Mwanafunzi Bora wa Astashaada ya Uongozaji watalii na uwindaji wa kitalii. Wanafunzi hawa wote wamekuwa pia wakishiriki katika shughuli za kijamii na kitaaluma kama vile klabu, vikundi, na miradi mbalimbali.



Katika kategoria za Uongozi Bora ndani ya Serikali ya Wanafunzi (SUASO), viongozi mbalimbali wamepewa tuzo kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kwa manufaa ya wanafunzi. Leha Naftar Josephat, ambaye ameshinda Tuzo ya Katibu Mkuu Mtendaji, amekuwa akisimamia shughuli zote za SUASO na kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata huduma bora na za haraka. Julius Elisha, ambaye ameshinda Tuzo ya Kamishina wa Elimu na Mikopo, amekuwa akisaidia wanafunzi katika masuala ya kitaaluma na kifedha, kama vile kufuatilia matokeo, kusuluhisha migogoro, na kushughulikia mikopo na ruzuku.



Mercy Magidanga, ambaye ameshinda Tuzo ya Afya, Chakula, na Mazingira, amekuwa akijihusisha na kuboresha hali ya afya, lishe, na usafi wa wanafunzi, kama vile kusimamia huduma za kantini, na takataka. Nelly Uswege na Victor Urio, ambao wameshinda Tuzo ya Usimamizi wa Mabweni kwa Wanawake na Wanaume mtawalia, wamekuwa wakiwahudumia wanafunzi wanaoishi katika mabweni ya kampasi.

# Mizengo Pinda Campus Celebrates Graduates at the 42nd Sokoine University of Agriculture Graduation Ceremony




The Mizengo Pinda Campus shone brightly at the 42nd Sokoine University of Agriculture (SUA) Graduation Ceremony on Thursday, November 23rd, 2023, at the Edward Moringe Campus in Morogoro. The ceremony saw the Chancellor of SUA, Hon. (Rtd.) Justice Joseph Sinde Warioba confer the degree and non-degree awards to a graduating class filled with talented and dedicated individuals.



A total of 46 students graduated with Bachelor of Science degrees in Bee Resource Management, nine earned Diplomas in Crop Production and Management, and another nine received Certificates in Tour Guide and Hunting Operations. These achievements reflect the diverse and robust academic programs at the Mizengo Pinda Campus.

One of the ceremony's highlights was the recognition of Vaileth Franc Chiwango, who was named the best student across the entire Sokoine University of Agriculture for 2023. This accolade underscores the commitment of the Mizengo Pinda Campus to academic excellence and the nurturing of a supportive learning environment.

The Mizengo Pinda Campus offers a diverse range of programs tailored to meet the needs of today's workforce. The Bachelor of Science in Bee Resource Management program imparts graduates with the necessary skills and knowledge to manage bee resources effectively and sustainably, thereby contributing to the growth and development of the apiculture industry. The Diploma in Crop Production and Management program provides graduates with valuable practical skills and knowledge vital to excelling in the agricultural sector, ensuring food security, and promoting rural development. Finally, the Certificate in Tour Guide and Hunting Operations program prepares graduates to become competent and knowledgeable professionals in the tourism industry, promoting Tanzania's rich natural resources and cultural heritage to visitors worldwide.



The Mizengo Pinda Campus is a place where future leaders and professionals are cultivated with passion. With a strong emphasis on academic excellence, a nurturing learning environment, and diverse program offerings, our graduates are equipped to impact society and contribute to the nation's development positively. Our commitment to empowering students to achieve their full potential and make a meaningful difference in the world is sincere and unwavering.

# APIARY APPRENTICESHIP: VILOLO'S HIVE CLEANING AND INSECT REMOVAL EXERCISE

Students of the first degree in bee resource management in the second year doing an exercise to clean and remove insects from the hives in the bee farm of the University of Sokoine Agriculture, the Pinda hives campus of Mizengo Pinda located in Vilolo in the Katavi Region.







## Mafanikio ya Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) katika Kampasi ya Mizengo Pinda, Mkoa wa Katavi

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Profesa Raphael Chibunda, amefanya ziara katika Kampasi ya Mizengo Pinda, Mkoa wa Katavi. Lengo la ziara hii lilikuwa kusikiliza kero na changamoto za watumishi, pamoja na kujionea maeneo ambayo yatakwenda kujengwa majengo matatu kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET). Majengo hayo ni Jengo la Taaluma, Bwalo, na Dhaaria.



Katika ziara hiyo, Profesa Chibunda aliwahimiza watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda kushirikiana katika kazi na kuendeleza utamaduni wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ili kuwa mfano wa kuigwa kwa jamii inayowazunguka.



Mratibu wa Mradi wa HEET, Dkt. Winfried Mbungu, alitoa taarifa kuhusu maendeleo ya mradi huo. Kampasi ya Mizengo Pinda itajengewa majengo matatu: Jengo la Taaluma, Bwalo, na Dhaaria. Dkt. Mbungu aliwathibitishia watumishi wa kampasi kuwa mradi huo utakamilika kwa wakati uliokusudiwa.

Mradi wa HEET unadhamini mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Dkt. Mbungu aliwahimiza watumishi kutumia fursa hiyo kujiendeleza kielimu. Baadhi ya watumishi wamepata udhamini wa kielimu kupitia mradi huo.

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kinajivunia maendeleo haya katika Kampasi ya Mizengo Pinda



Katika kuendeleza mafanikio ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Makamu Mkuu wa Chuo Utawala, Mipango, na Fedha, Profesa Amandus Muhairwa, ametoa maagizo muhimu kwa watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda, Mkoa wa Katavi. Hapa ni muhtasari wa maagizo hayo:

Matumizi ya Ofisi: Profesa Muhairwa amewataka watumishi kutumia vyema ofisi zao wanapokabiliwa na changamoto au wanapohitaji ufafanuzi wa taarifa zinazowahusu. Hakuna haja ya kuogopa ofisi hizo; badala yake, watumishi wanapaswa kuzitumia kwa ufanisi.

Stahiki za Wafanyakazi: Wafanyakazi wote wanaodai stahiki zao watapata. Profesa Muhairwa amewahimiza watumishi kufika katika ofisi husika ili kupata taarifa kamili kuhusu masuala yao.

Utaratibu wa Kufika Ofisini: Profesa Muhairwa amesisitiza umuhimu wa kuwai ofisini ili kufanya kazi kwa weledi na kutimiza vyema majukumu yao kama watumishi wa umma. Kufika ofisini kwa wakati ni sehemu ya kuimarisha utendaji na kutoa huduma bora kwa jamii.

Kwa kufuata maagizo haya, watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda wataweza kuchangia katika ufanisi wa chuo na kuleta mabadiliko chanya katika jamii inayowazunguka.



Katika kuhakikisha ubora wa elimu na kuzalisha wataalamu wenye tija, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) anayeshughulikia Taaluma na Utafiti, Profesa Maulid Mwatawala, ametoa maagizo muhimu kwa wana Taaluma. Hapa ni muhtasari wa maagizo hayo:

Ufundishaji Bora: Profesa Mwatawala amewakumbusha wana Taaluma kuzingatia misingi ya ufundishaji. Wanapaswa kufuata utamaduni, utaratibu, na muongozo wa chuo katika kufundisha ili kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora na kuwa wataalamu wazuri.
Kuboresha Mtaala: Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kipo katika zoezi la kuboresha mtaala wake. Kampasi ya Mizengo Pinda imejikita katika kuongeza baadhi ya kozi ili kuongeza idadi ya wanafunzi katika kampasi hiyo. Hatua hii itachochea maendeleo ya kiuchumi katika jamii inayozunguka chuo na mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.
Kwa kufuata maagizo haya, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kitaendelea kutoa wataalamu walioandaliwa vyema na kuwa mstari wa mbele katika kuleta maendeleo katika taifa letu.

## SUA, Kampasi ya Mizeingo Pinda, Yashiriki Kikamilifu katika Maonyesho ya 30 ya Nane Nane, Yavutia Wageni Zaidi ya 300




Katika Maonesho ya 30 ya Nane Nane yaliyofanyika kitaifa katika viwanja vya John Mwakangale, mkoani Mbeya, baadhi ya watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda walishiriki kikamilifu. Watumishi hao walionyesha baadhi ya bidhaa zinazozalishwa na wanafunzi wa kampasi hiyo, kuonyesha mchango wao katika sekta ya kilimo, biashara na uvumbuzi. Hii ni hatua muhimu katika kukuza na kutangaza uzalishaji wa ndani na kushirikiana katika maendeleo ya kilimo na biashara nchini Tanzania.



Maonesho hayo yalifanyika kuanzia Agosti 1 hadi Agosti 10 2023, na yalihusisha mataifa zaidi ya thelathini kutoka sehemu mbalimbali. Na Kaulimbiu ya maonesho hayo ilikuwa: **"Vijana na Wanawake ni Msingi Imara wa Mfumo Endelevu wa Chakula."** Hii inaendana na mkutano wa jukwaa la mifumo ya chakula Afrika (Africa Food Forum) uliofanyika Jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 5 hadi 8 Septemba 2023.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mheshimiwa Juma Homera, alieleza kuwa maonesho hayo yalifunguliwa na Makamu wa Rais, Dkt. Philip Isdory Mpango, na kufungwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. "Ni matumaini kuwa maonesho haya yatasaidia kuhamasisha kilimo bora, kukuza biashara, na kuwawezesha vijana na wanawake katika mfumo endelevu wa chakula" alisema Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa.




Pia Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, pamoja na Katibu Mkuu wake, Profesa Calorline Nombo, walipata fursa ya kutembelea banda la maonesho la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo katika Kampasi ya Mizengo Pinda katika viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya



**Picha kushoto:** *Prof. Adolf Mkenda (Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia) akizungumza na Prof. Jeremiah Makindara.* **Picha kulia:** *Mwanafunzi wa shahada ya awali katika usimamizi wa rasilimali nyuki Ndg. Naftari Leha akizungumza na Prof. Adolf Mkenda.*

Hii ni hatua muhimu katika kukuza elimu na teknolojia nchini Tanzania. Kupitia maonesho hayo, wanafunzi na watafiti wanaweza kujifunza na kushirikiana katika kuboresha sekta ya kilimo na maendeleo endelevu. Ni matumaini yetu kuwa Tanzania itaendelea kufanya maendeleo makubwa katika elimu na sayansi ili kuchangia katika ukuaji wa taifa

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mheshimiwa Mwanamvua Mrindoko, pia alifika katika banda la letu la Kampasi ya Mizengo Pinda. Hii inaonyesha umuhimu wa kujifunza na kushirikiana katika kukuza elimu na maendeleo katika mkoa wa Katavi na mikoa ya nyanda za juu kusini.



**Picha kushoto:** *Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mheshimiwa Mwanamvua Mrindoko akizungumza na afisa udahili wa kampasi ya Mizengo Pinda ndugu Abel Lugimba pamoja na afisa kilimo ndugu Alphonce Tambalu.* **Picha kulia:** *Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa akizungumza na Kaimu Mkuu wa Idara ya Usimamizi na Uhifadhi wa Maliasili Ndg. Evaristus Magani.*

Mheshimiwa Majid Hemed Mwanga, Mkuu wa Wilaya ya Mlele, naye alijitokeza kwenye banda la Kampasi ya Mizengo Pinda wakati wa Maonesho hayo. Lengo lake lilikuwa kujionea na kujifunza kuhusu bidhaa zinazozalishwa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Kampasi ya Mizengo Pinda.

"Viongozi na wananchi wanathamini sana elimu na maendeleo, na wanafurahia kushiriki katika hafla kama hizi ili kukuza maarifa na ujuzi katika jamii. Ni matumaini yangu kuwa juhudi hizi zitaleta tija na kuchangia katika maendeleo ya wilaya na mkoa kwa ujumla" alisema Mkuu wa Wilaya ya Mlele Mhe. Majid Hemed Mwanga




***Picha kushoto:** Mheshimiwa Majid Hemed Mwanga, Mkuu wa Wilaya ya Mlele akizunguza na mwanafunzi wa shahada ya awali katika sayansi ya usimamizi wa rasilimali nyuki. **Picha kulia:** Mheshimiwa Mkuu wa wilaya akiwa katika picha ya pamoja na watumishi na wanafunzi wa Kampasi ya Mizengo Pinda.*

Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Mheshimiwa Solomon Itunda, amepata fursa ya kutembelea banda la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) katika maonesho ya Nanenane yanayofanyika kitaifa katika viwanja vya John Mwakangale, Mkoani Mbeya.




*Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Mheshimiwa Solomon Itunda akiwa katika banda la Kampasi ya Mizengo Pinda*

Viongozi wengine walioitembelea kampasi hii ni pamoja na Dr. Elirehema J. Doriye, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima ya Taifa (NIC Insurance), Mkuu wa kitengo cha kilimo Bank ya Azania ndugu Agustino Matutu, Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Sukari Tanzania, Profesa Kenneth Bengesi. Wengine ni Dkt. Florens Turuka, ambaye ni Mtumishi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Mshauri wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu masuala ya chakula na kilimo pamoja na Bwana Rodrick Lazaro Mpogolo ambaye ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya.






***Picha kushoto***: *Dr. Elirehema J. Doriye, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima ya Taifa (NIC Insurance) akizunguza na Prof. Jeremiah Makindara.* ***Picha kulia***: *Mkuu wa kitengo cha kilimo Bank ya Azania ndugu Agustino Matutu akipokea kipepelushi kutoka kwa Naibu Rasi wa Ndaki Kampasi ya Mizengo Pinda katavi Prof Jeremia Makindara.*





***Picha kushoto***: *Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Sukari Tanzania, Profesa Kenneth Bengesi akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda.* ***Picha kulia***: *Dkt. Florens Turuka akiwa katika picha na wanafunzi wa Kampasi ya Mizengo Pinda.*





*Bwana Rodrick Lazaro Mpogolo, Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, akiwa pamoja na watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda katika banda la maonyesho ya nane nane.*

## MPC KATIKA MICHEZO

Chuo Kikuu Cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Kampasi ya Mizengo Pinda Mbali na kufundisha, kufanya tafiti, kutoa ushauri wa kitaalamu na uzalishaji mali katika nyanja za kilimo, mifugo, maliasili na utalii. watumishi na wanachuo ushiriki katika mambo mbalimbali ya kijamii kama kuchangia damu,michezo,Warsha na Makongamano.




Katika picha ni Baadhi ya wachezaji wa Timu ya Watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda walipokwenda kucheza mchezo wa kirafiki na timu ya Maveterani ya Majimoto iliyopo ndani ya Halmashauri ya Mpimbwe,Mkoa wa Katavi.Mchezo wenye lengo la Kuboresha Afya na Kujenga Urafiki.








*Timu ya wanafunzi ya mpira wa pete ya shahada ya awali ya sayansi ya usimamizi wa rasilimali nyuki*



*Timu ya wanafunzi ya mpira wa pete ya astashahada ya uongozaji watalii na uwindaji wa kitalii*

## Wahariri


**Mhariri Mtendaji** - Bw. Joseph Ruboha
**Mhariri Mkuu** - Bi. Suzana Magobeko
**Waandishi** - Bw. Edson Kanisa
Prof. Jeremiah Makindara


## Limetolewa na:


Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo
Kampasi ya Mizengo Pinda
S.L.P 82, Mpanda, Katavi
34 SITALIKE RD
50318 KIBAONI, MLELE
Barua pepe: principalmpc@sua.ac.tz





